

---

ERICK KABERWA,  
S.L.P 145,  
BUKOBA.  
20/04/2024.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI,  
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI,  
UCHAGUZI HOUSE,  
ENE LA UWEKEZAJI NJEDENGWA,  
KITALU D, KIWANJA NA. 4,  
5 BARABARA YA UCHAGUZI,  
S.L.P 358,  
**41107 DODOMA.**

**YAH: OMBI LA NAFASI YA KAZI YA MWENDESHAVIFAA VYA  
BIOMETRIKI/MWANDISHI MSAIDIZI.**

Rejea somo tajwa hapo juu,

Mimi ni kijana mtanzania mwenye umri wa miaka 33 ni mkazi wa kata ya Rwamishenye halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Elimu yangu ni shahada ya kwanza. Katika tangazo lilitolewa na Ofisi yako tarehe 15/04/2024 napenda kuomba nafasi ya kazi ya mwendesha vifaa vya Biometriki/Mwandishi msaidizi, nina uwezo mzuri wa kutumia kompyuta pamoja na simu janja hata hivyo nina uzoefu na kazi hiyo kwani mnamo mwaka 2020 nilifanya kazi hiyo katika Kata ya Rwamishenye.

Pamoja na barua hii pia nimeambatanisha picha zangu ndogo mbili, wasifu wa maelezo yangu binafsi (CV), vivuli vya vyeti vyangu vya taaluma na kuzaliwa pamoja na barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa mtaa ninakoishi.

Natumai ombi langu litapokelewa na kufanyiwa kazi.

Wako katika ujenzi wa taifa,

.....  
ERICK KABERWA,  
0766 778 754  
Email: nijuzehabariblog@gmail.com